Hadithi Ndani Ya Kanisa (Fables In The Church)

Na

Ellis P. Forsman

Hadithi Ndani Ya Kanisa

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 26, 2011

Hadithi Ndani Ya Kanisa

Siyo yote yanayopita kwa ajili ya ukweli katika mimbari, nyaraka za kidini, na katika barua pepe miongoni mwa Wakristo ni za kweli kulingana na Biblia, bali ni hadithi.

"Nini? Hadithi katika kanisa?" unauliza. "Hadithi katika makanisa mengine, lakini yawezekana sio katika kanisa la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo!"

Hadithi hizi hazijaribu kuja katika kanisa la Kristo chini ya utambulisho wa hadithi, lakini badala yake kama ishara katika ukweli ili kutangaza wazo Fulani. Wazo lililozoeleka la dini nyingi ni matumizi ya hadithi katika kufundisha na kushinikiza mtazamo wa maadili na Nyanja za dini kwa muundo ambao ni rahisi kusimilisha na kukumbuka. Hadithi siyo mafundisho mazuri. Hazitokei pasipo mkusanyiko wa umbo, yasiyonyooka, na hasa tafsiri zisizo na maana. Inakataa na kuacha maneno mengi ya wazi ya Mungu ili kuanzisha mafundisho ambayo si ya kweli. Kusudi lo lote ambalo mtoaji analo la kutoa hadithi kama hiyo, bila kujali hisia ya moyo wanayotoa, matumizi ya hadithi kama hizo ni kinyume na agizo la Mungu.

Bwana wetu ametoa maandiko yafuatayo kama onyo dhidi ya matumizi hayo:

- 1 Tim. 1:4, "*Wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani; basi ufanye hivyo.*"
- 1 Tim. 4:7, "*Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae nawe ujizoeze kupata utauwa.*"
- 1 Tim. 6:20, "*Ee Timotheo ilinde hiyo amana ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo;*"
- 2 Tim. 2: 16, "*Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu.*"
- 2 Tim. 4:4, "*Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*"
- Tito 1:14, "*Wasisikilize hadithi za Kiyahudi, wala maagizo ya watu wajiepushao na yaliyo kweli.*"

Wasioamini wanaweza kusema kwamba msingi wetu wa imani ni hadithi, lakini tunafahamu tofauti. Matukio katika kuzaliwa kwa Bwana wetu, ukuu, uhai, kufa, kuzikwa, na kufufuka siyo hadithi. 2 Pet. 1:16, "*Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu,*

tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake."

Wakristo hawatakiwi kutumia silaha za hadithi za ujanja ili kudumisha imani yao katika mpango wa Mungu wa wokovu; wanapaswa kutumia mpango wa Mungu wa wazi na maneno rahisi ili kutimiza hili. Kwa miaka, kauli mbiu ya kanisa la Kristo imekuwa, "Nena pale Biblia inaponena, na kaa kimya Biblia ilipo kaa kimya." Kwa miaka ya hivi karibuni Shetani amejipenyeza katika kanisa lisilolindwa na kugeza mawazo ya wengi kukubali hadithi kama hizo.

Mtu anaingiaje kwenye hadithi? Inaonekana kufuata matakwa yetu wenyewe ili kuamini mambo kama hayo. Wengine wanachoshwa na mafundisho ya wazi ya Biblia na masikio yao "yanawasha" wanaposikia kitu ambacho hawajawahi kusikia kabla; ghafla ujumbe unakuwa wa kuvutia tofauti na ilivyokuwa awali. Wahubiri wanapoona mwitikio na faida wanayopata wanapotumia "*hadithi zilizo jaa uongo*", wanatiwa moyo kuzidi kuzitumia zaidi. Hataivyo, matokeo, ni kwamba Wakristo wengi ambao hawahoji wanachofundishwa wanakubali hadithi hizi na mambo mengine ya upuuzi katika kanisa sambamba na ukweli wa Biblia.

Tiba dhidi ya hadithi kama hizo na mambo mengine ya upuuzi katika makanisa ni kuwafundisha watu wa Mungu kuhusu maonyo ya biblia katika kutumia upanga wake war oho katika neno lake la kweli badala ya maneno ya upuuzi yenye mashaka. Hadithi hazitokani na mafundisho ya mitume, bali za Shetani. Mungu haruhusu matumizi ya ujanja ujanja (hadithi). Bwana wetu anatuonya kwa maneno yafuatayo:

- Mat. 4:4, "*Naye akajibu akasema, imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tuu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*"
- Ayu. 28:28, "*Kisha akmwambia mwanadamu, tazama kumcha Bwana ndiyo hekima, na kujitenga na uovu ndiyo ufahamu.*"
- Efe. 5:10, "*Mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.*"
- 1 Thes. 5:21-22, "*Jitengeni na ubaya wa kila namna. Mungu wa amani mwenyewe awatakase nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*"

- 1 Yoh. 4:1, "*Wapenzi msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*"

- 2 Tim. 4:1-4, "*Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake*; *lihubiri neno; uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*"

- Gal. 1:8-9, "*Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa nasema, tena mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe.*"

Paulo alimuonya Timotheo mara nyingi kwamba asisubutu kwenda hata katika njia ya kutumia uongo kama inavyopingwa kutumia mafundisho ya uzima. Hataivyo, inaweza kuwa hadithi "adilifu", kama siyo ya neno la Mungu basi ni kinyume. Hata kama kutumia hadithi katika kutangaza neno la Mungu inawapa wanaosikia faida, kwa ukweli inatenda kinyume. 2 Tim. 4:3-5, "*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza huduma yako.*" Kiukweli hadithi hudhoofisha neno la Mungu kwa kuwavuta watu katika hadithi. Watu wanataka njia mpya na zinazovutia kusikia injili; lakini hatupaswi kuigeukia ujumbe wa Shetani kwa uvuvio. Ndugu na dada, Bwana wetu anasema wakati utafika ambapo hayo yatatokea; wakati huo ndio sasa.

Tunaposoma Maneno ya Mungu Matakatifu ni zoezi la utauwa. Inahitajika juhudi katika kusoma Biblia "kama ilivyo" na kujionyesha wenyewe "tumekubaliwa" na Mungu kwa kulisoma. Kusoma hadithi inahitaji juhudi kidogo na ndio njia moja wapo ambayo Wakristo wanafanywa wavivu na Shetani wale wasiofanya juhudi kuthibitisha kinachokubalika na Bwana.

Zifuatazo ni mifano ambazo nimepokea au kusikia ambazo zinaweza kutajwa kama hadithi. Mengi ya hizi yametokana na

matumizi ya barua pepe na usahihi au ukweli ambao unaweza kuthitishwa kwa msaada wa mtandao wa Snopes.com.

Siku iliyopotea inadai. Labda wanasayansi wa NASA waligundua "siku iliyopotea" kwa wakati ambao inajibu kwa hesabu za Kibiblia ya jua kusimama angani kama inavyoonekana katika Yoshua 10:12-13. Wakati Wakristo wanaamini Biblia, matukio katika NASA hayakutokea.

Filamu ya Gay Yesu inadai. Madai haya yalifanywa na baadhi kwamba katika mwaka 2001 filamu ingetolewa inayomwonyesha Yesu na wanafunzi wake kama basha. Juhudi za barua pepe zilikwenda nje zikihamasisha kila mmoja atume ujumbe kwa Mwana Sheria Mkuu wakimwomba kwamba utoaji wa filamu hii isitishwe. Ofisi hii ilijawa na barua na barua pepe. Baadhi ya barua pepe zilizo fanana zilikuwa katika ofisi ya mwanasheria mkuu wa Illinois, na yenyewe pia ilijaa. Ofisi ya Illinois ilitoa ombi kwa jamii kupitia jarida la Ann Landers ili wasitishe haditi hii ya uongo. Hata leo ofisi hii inapokea kadiri ya pingamizi 1000 kila wiki. Hoaxes kufa kwa ujasiri. Hataivyo kulikuwa na mchezo uliopewa jina la "Corpus Christi" iliyoonyesha Yesu Kristo na Wanafunzi wake katika mwanga huu.

Mikono ya Mungu inadai. Picha ya muundo wa wingu katika kimbunga mwaka wa 2004 ulikusanyika ukionyesha mikono ya Mungu ukiwa umenyooshwa juu ya maangamizi. Picha kama hii iliviringishwa mwaka wa 2007 kwa madai kwamba ilichukuliwa Kentucky na pia Texas, alafu pia 2010 ikisema ilichukuliwa kutokana na maangamizi ya tetemeko la ardhi ya Haiti. Ilitumiwa kama uvuvio wa Mungu anavyowajali wanadamu. Mtandao huu wa Snopes unathibitisha kwamba picha ilitengenezwa ili kufanya mawingu yaonekane kama mikono ya Mungu.

Mwamba wa Ajabu anadai. Picha iliyodaiwa kuwa ya mwamba chini ya bahari huko Birmania wakati maji yaliyokamilika yakitulia ukiigeuza upande wake inaonyehsa umbo unapoitazama mwamba unaona mama anayeomba na mtoto. Umbo ilikuwa itoe utulivu kwa mtazamaji. Hakika picha hii ilichukuliwa kutoka katika mchoro wa mkono.

Yesu katika wingu anadai. Rubani wa dege za kivita alipiga picha wakati wa vita Korea. Muda mfupi baada ya kujitengenezea njia katika *Gazeti Linalojitegemea la kila siku* na andiko hili "Yesu katika mawingu". Kimsingi picha hii ilionyesha umbo la Yesu akimuangalia rubani wa Kimarekani. Kulikuwa na nukuu katika gazeti kutoka kwa rubani akisema picha iliwainua kiroho. Kwa haraka picha hii ikasambaa kila sehemu ya Amerika kama uvuvi ya juhudi za vita. Wakati picha halisi ilipatikana katika mwaka wa

1951 iligundulika kwamba umbo la Yesu lilichorwa. Picha hii ilikuwa ya uongo.

Uokoaji wa Kimalaika Anadai. Kimsingi katika mwaka wa 2000, mwili wa mwanamke aliyekufa kwenye ajali ya gari unawaongoza waokoaji katika uharibifu kumwokoa mtoto wake aliyekuwa hai ndani ya gari lile. Misho wa hadithi hii inamtia moyo wasomaji waamini katika miujiza ndani ya maisha yao pia. Snopes anasema mila iliyozoeleka inaelezewa na mkusanyiko huu kwamba ni mawazo tu ya mwandishi; wengine wakishughulika na uwepo wa Kristo na Roho Mtakatifu wakiwalinda wapendwa na hatari. Ifuatayo ni mojawapo:

Alley Oops anadai. Labda, binti wa Kikristo anayeomba kwa ajili ya ulinzi akielekea nyumbani akiwa amechelewa wakati wa usiku anaokolewa na malaika wawili wanaomlinda asikutane wana wabakaji. Binti mwingine alibakwa katika alley kama hiyo dakika 20 baada ya binti huyu kupita baada ya hadithi hii kutengeneza historia binti “aliyelindwa” akapita mbele na kumwambia polisi hadithi yake; kwamba angeweza kumtambua mtu aliyemwona katika alley. Baada ya kumtambua mbakaji kwenye msitari akamwuliza kwa nini alimruhusu apite katika alley bila kuguswa. Mtu yule akamwambia binti, “Kwa sababu kulikuwa na wanaume wawili wakitembea naye.”hadithi inampa msomaji wake uvuvio wa kuomba. Hataivyo, nyaraka tofauti ya hadithi hii zimekusanywa tangu mwaka wa 2001. Hakuna majina au sehemu zinazoonyeshwa katika hadithi yo yote. Snopes anasema hizi ni hadithi za kutunga katika mitandao. Tukio hili haliwahi kukutwa katika ripoti ya kipolisi.

Ndugu na dada, kuna uchafu mwingi wa kidini katika mtandao! Na wasomaji wanatiwa moyo kuwatumia wengine katika orodha zao za barua pepe.

Ushauri kutoka kwa Snopes.com:

“Wakati wo wote unapoona barua pepe inayosema watumie marafiki zako “10”, tia sahihi hapa, au utapata bahati mbaya, bahati nzuri, au vyovyote, mara nyingi zina anwani zilizoshikanishwa inayopeperusha mawasiliano na barua pepe za wale unaowatumia.”

Kol. 2:8, “*Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.*”

Kiukweli natarajia hii imekuwa msaada kwako.